JESMA 007

# JARIBIO LA SABA K.C.P.E
## DARASA LA NANE 2022

KISWAHILI
SEHEMU YA
KWANZA:
LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Katika karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** Buda ni kwa ajuza ilhali beberu ni kwa
   A. kikwara
   B. mtamba
   C. mbarika
   D. mtelea

Jibu sahihi ni C (mbarika)

**1** [A] [B] [C] [D]   **11** [A] [B] ▬ [D]   **21** [A] [B] [C] [D]   **31** [A] [B] [C] [D]   **41** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

Tovuti: www.jesmapublishersltd.com  Barua pepe: jesmapublishers@yahoo.com



KISWAHILI LUGHA

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.*

___1___: hulka ya mtoto ___2___ na matendo ya wale walio na mamlaka ___3___. Kwa hivyo, ___4___ tu kumshauri mtoto kufuata mienendo ifaayo. ___5___ yenyewe itakuwa na maana tu ___6___ inaambatana sambamba na yale ___7___ na washauri. Wanajamii hawana budi ___8___ mienendo yao ili iambatane na maadili ya kijamii.

1. A. Ukibebwa usilevyelevye miguu B. Mtoto akibebwa hutazama kisogo cha nina C. Nazi mbovu ni harabu ya nzima D. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo
2. A. huathirika B. huadhiriwa C. huadhirika D. huathiriwa
3. A. juu yake B. dhidi yake C. miongoni mwao D. kati yake
4. A. inatosha B. ingetosha C. haitoshi D. isingetosha
5. A. Nasaha B. Nyaadhi C. Ushauri D. Usia
6. A. ilhali B. madamu C. kwani D. iwapo
7. A. wanayotenda B. yanaotendewa C. yanayotendwa D. wanaotenda
8. A. kupiga darubini B. kuipiga msasa C. kutia fora D. kutia kapuni

Maisha yangu yalifungua ukurasa mpya ___9___ na shule ya Makinika. Kwa nyota ya jaha ___10___ mdhamini aliyejitolea kugharimia masomo yangu. Bibi yule mwenye ___11___ aliamua kunisaidia ingawa ___12___. Katika hali hiyo, nilizamia elimu kwa ___13___ kuu ___14___ sikutaka kuipoteza nafasi hii ya ___15___ niliyotunukiwa na Karima.

9. A. nilipojiunga B. nilikojiunga C. nilivyojiunga D. niliyojiunga
10. A. ningekuwa nimempata B. nilikuwa nikimpata C. nimekuwa nikimpata D. nilikuwa nimempata
11. A. mkono birika B. mkono mwepesi C. mkono wazi D. mkono mzito
12. A. hakunihusu ndewe wala sikio B. hatukuhusiana kwa damu wala usaha C. nilijitia kati kama mchuzi D. nilijikaukia kama ukuni
13. A. ari B. hari C. adha D. matumaini
14. A. : B. ; C. ___ D. ”
15. A. upekee B. pekee C. kipekee D. kipweke

*Kuanzia swali la **16** mpaka **30**, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.*

**16.** Chagua sentensi ambayo ni muungano sahihi wa sentensi zifuatazo.
Kamau hakuenda kwake. Kamau ameonana naye.
A. Lau Kamau hakuenda kwake hakuonana naye.
B. Endapo Kamau angeenda kwake angeonana naye.
C. Minghairi ya Kamau kuenda kwake ameonana naye.
D. Kamau ameonana naye licha ya kutoenda kwake.

**17.** Cheka ni kwa meheshi kama ilivyo **dhulumu** kwa
A. dhuluma  B. udhalimu
C. mdhalimu  D. dhalimu.

**18.** Andika kwa umoja wa sentensi ifuatayo.
**Nyufa zilizokarabatiwa zimepasuka tena.**
A. Nyufa iliyokarabatiwa imepasuka tena.
B. Unyufa uliokarabatiwa umepasuka tena.
C. Ufa uliokarabatiwa umepasuka tena.
D. Ufa uliyo karabatiwa umepasuka tena.

**19.** Bainisha matumizi ya **ki** katika sentensi ifuatayo.
**Mjomba alitembea kijeshi akienda sokoni.**
A. Namna, wakati.
B. Namna, masharti.
C. Wakati, hali.
D. Wakati, masharti.

**20.** **Kikosi** ni mkusanyiko wa askari zaidi ya elfu moja. **Kikosi** pia ni
A. sehemu ya nyuma ya shingo
B. kikundi cha watu watembeao pamoja
C. Aina ya pambo la mkononi au mguuni
D. Nguo yenye upindo wa rangirangi ivaliwayo kiunoni

**21.** Chagua sentensi iliyo na matumizi sahihi ya kirejeshi **-o** tamati.
A. Wageni ambao wajao wametoka bara.
B. Wageni wakujao wametoka bara.
C. Wageni wanaokuja wametoka bara.
D. Wageni wajao wametoka bara.

**22.** Neno **kiamshakinywa** lina silabi ngapi?
A. 6  B. 5
C. 7  D. 11

**23.** Kuku ni kwa kizimba, **mchwa** ni kwa
A. zeriba.
B. kifukofuko.
C. kidurusi.
D. kombe.

**24.** Andika kauli ya **kutendewa** ya sentensi hizi:
**Jilo aliyasoma makala. Jilo alikuwa maktabani.**
A. Jilo alisomewa makala maktabani.
B. Makala yalisomewa maktabani na Jilo.
C. Makala yalisomwa na Jilo maktabani.
D. Jilo alisomea makala maktabani.

**25.** Msemo **amekaa tutwe** una maana gani?
A. Kaa maisha ya kujitenga na watu.
B. Kuwa katika hali ya tahadhari.
C. Kukaa pasi na mpango, yaani ovyoovyo.
D. Kaa bila kusema au kufanya lolote.

**26.** Orodha ipi ina **vielezi** pekee?
A. Kando ya, zaidi ya, pembeni, katikati.
B. Taratibu, mjini, jana, tena.
C. Licha ya, aghalabu, japo, mithili ya.
D. Angalau, asteaste, haraka.

**27.** Andika usemi wa taarifa wa sentensi ifuatayo:
**Kaka kiondoka mapema utafika kabla ya mkutano.**
A. Kaka alimwambia kuwa iwapo angeondoka mapema angefika kabla ya mkutano.
B. Kaka alimwahidi kuwa akiondoka mapema atafika kabla ya mkutano.
C. Kaka aliagizwa kuondoka mapema ili afike kabla ya mkutano.
D. Kaka aliambiwa kuwa iwapo angeondoka mapema angefika kabla ya mkutano.

**28.** Kiambishi **tu** katika neno **tuliandikiwa** kinaonyesha
A. mtenda.
B. mtendwa.
C. mtendewa.
D. kitendo.

**29.** Chagua sentensi iliyo katika hali ya kuagiza.
A. Iwapo utamsikiliza utamwelewa zaidi.
B. Mpeleke mtoto kwa daktari akatibiwe.
C. Lo! Kumbe umealikwa pia?
D. Tafadhali nisaidie kuuinua mzigo huu.

**30.** Chagua jozi ya methali zenye maana sawa.
*i) Lisilo dawa haliangaliki.*
*ii) Lisilo mkoma, hujikoma lilo.*
*iii) Cha kuvunda hakina ubani.*
*iv) Changu ni bora kuliko chetu*
*v) Jahazi la mkuta haliendi joshi.*
A. (i), (ii)  B. (iii), (iv)
C. (i), (v)  D. (i), (iii)

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali kuanzia nambari* **31** *mpaka* **40**

"Mgeni mheshimiwa, Bwana Ustadh, mwalimu mkuu Bwana Safari, Naibu wa mwalimu mkuu, walimu, viongozi mbalimbali wa wanafunzi, mabibi na mabwana, hamjambo? Namshukuru mwalimu mkuu kwa kunipa fursa hii kulizungumzia kongamano hili.

Wanafunzi wenzangu, kama mjuavyo hii ndiyo mara yangu ya mwisho kutoa mazungumzo yangu rasmi kama rais wa serikali ya watoto humu shuleni. Hata tunapoitilia nanga safari yetu ya masomo humu shuleni, ni muhimu kuangazia mafanikio na changamoto ambazo tumepitia. Mgeni mheshimiwa, ningependa kuishukuru ofisi yako ya Hazina ya ufadhili kwa mchango iliyoipa shule yetu katika kipindi cha miaka minane iliyopita. Wanafunzi wenzangu, mtakumbuka kwamba tulipojiunga na shule hii ya Angazambele hamkuwa na madarasa. Kumbukeni tulikuwa tukisomea chini ya mbuyu ule. Kumbukeni tulivyofurahi darasa la kwanza na la pili lilipojengwa. Hivi sasa wanafunzi wanaanza kujifunza kutumia tarakilishi wakiwa katika darasa la kwanza. Haya yote yamewezekana kwa ushirikiano kati ya Mwalimu mkuu, Wizara ya Elimu na Hazina ya Ufadhili.

Mgeni mheshimiwa, hata mimi na wenzangu **tunapokunja jamvi letu katika shule hii,** sina budi kuwashukuru wanafunzi wenzangu kwa kujitolea mhanga kufanikisha maendeleo shuleni. Tuna mengi ya kujivunia kama waanzilishi wa shule hii. Tumefanya kazi bega kwa bega na walimu kudumisha nidhamu si katika shule yetu tu bali pia katika ujirani wa shule. Na isidhaniwe ni darasa la nane tu ambalo limechangia udumishaji wa nidhamu. La! Hasha! Shule nzima imekaa angekuchunguza na kuangamiza vichocheo vyote vya utovu wa nidhamu. Mathalani, juzi tumewasaidia polisi kumtia mbaroni ghulamu mwenzetu ambaye alikuwa ameanza kupenyeza dawa za kulevya shuleni. Hali kadhalika, wanafunzi wa gredi ya sita walishirikiana kuanzisha chama cha Mwenge ambacho kimejifunga kibwekwe kuzuia uharibifu wa mazingira.

**Mwenye macho haambiwi tazama**. Mgeni mheshimiwa, utakiri kwamba mandhari ya shule hii ni ya kumtoa nyoka pangoni. Tazama miti ile mibichi ambayo imekolea rangi ya kijani kibichi! Tazama mabustani yanayohanikiza harufu nzuri ya maua. Tazama mapipa ya kutupia taka yaliyotengenezwa kwa ustadi maalum na hawa hawa wanafunzi! Heko wenzangu!

Mwalimu mkuu, hata tunapoipa kisogo shule hii na kukabiliana na mustakabali ambao hatuna uhakika nao, sisi hatuna hofu kwani shule hii imetuandaa kikamilifu kupambana na vizingiti vya maisha. Tumefunzwa mikakati ya kuepuka mitego ya maisha. Tumefunzwa kuhusu umuhimu wa bidii na namna ya kupigania haki kwa njia chanya. Tumefunzwa umuhimu wa stahamala na kusameheana. Bi Nasaha, tunakushukuru kwa kutuelekeza kuhusu namna ya kufanya ushauri-rika. Hili limetufanya kuwaokoa wanafunzi wengine ambao walikuwa na matatizo ya kibinafsi na kifamilia. Tunatarajia kutumia maarifa uliyotupa kuwaelekeza wenzetu katika shule za upili.

Mgeni mheshimiwa, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, ningependa kuwashauri wanafunzi wenzangu wajikinge dhidi ya kupotoshwa na wengine. Ni dhahiri kwamba maovu mengi ambayo yanatendwa na binadamu hutokana na mazingira anapoishi. Ni muhimu tukumbuke kwamba jambo haliwi halali eti kwa sababu linatendwa na watu wote. Ni vyema kuwa na msimamo thabiti. Nawasihi nyote tuungane kutetea maadili ya jamii yetu hata kama wenzetu wote watatukimbia. Upo wakati mbapo mtu pweke hawi uvundo.

Mgeni mheshimawa, hata ninapotamatisha hotuba hii, ningependa kukushukuru kwa mawaidha uliyotupa. Nawatakieni nyote neema ya Mwenyezi Mungu. Asanteni."



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

31. Kulingana na aya ya pili,
A. ilikuwa mara ya mwisho kwa msemaji kutoa hotuba.
B. Mnenaji wa wenzake walipita raha na dhiki shuleni.
C. Mwandishi alisoma kwa msaada wa hazina ya ufadhili.
D. mkutano ulihudhuriwa na rais wa viongozi wa serikali.

32. Awali, katika shule ya Angazambele
A. wanafunzi walisomea chini ya mibuyu.
B. mlikuwa na madarasa mawili pekee.
C. mgeni wa heshima na wenzake walisomea chini ya mbuyu.
D. hali ya pale shuleni kwa jumla ilikuwa duni.

33. Kifungu **'tunapokunja jomvi letu katika shule hii'** kina maana kuwa
A. Msimulizi na mgeni wanakamilisha shughuli za mkutano shuleni.
B. Msimulizi na wenzake wanamaliza shughuli za mkutano shuleni.
C. Msimulizi, mwalimu mkuu na mgeni wanamaliza shughuli zao shuleni.
D. msimulizi na wenzake wanakamilisha masomo ya shuleni humo.

34. Msimulizi na wenzake wanajivunia yote haya ila
A. kuwa kigezo cha kuimarisha nidhamu katika jamii.
B. mchango wao katika kustawisha mazingira shuleni.
C. kupata ufanisi mkubwa katika mtihani wao.
D. kukabiliana na walinda usalama kukabiliana na uhalifu.

35. Methali, **'mwenye macho haambiwi tazama'** inasisitiza kuwa
A. mgeni anajionea mwenyewe namna mazingira yalivyotunzwa.
B. mgeni anaelewa waziwazi kuhusu ubora wa mazingira yanayotunzwa.
C. mgeni amesikia sifa za jinsi wanafunzi wanavyoyatunza mazingira.
D. mgeni anaona mazingira kote lau sivyo na shida ya macho.

36. Aya ya **nne** imebainisha kwamba,
A. maua hunawiri zaidi yanapopandwa shuleni.
B. wanafunzi wanaweza kutumia ubunifu kustawisha shule zao.
C. wanafunzi hutengeneza mapipa kwa ustadi zaidi kuliko yale ya dukani.
D. chama cha mwenge kilitengeneza mapipa na kupanda maua.

37. Shule imewaandaa wanafunzi vizuri kwani,
A. hawana uhakika kuhusu mustakabali wao.
B. hawataraji kupatana na pingamizi zozote maishani.
C. wamefunzwa stadi mbalimbali za maisha.
D. watajiunga na shule nzurinzuri za kitaifa.

38. Ushauri-rika umesaidia vipi shuleni?
A. Wanafunzi wamesaidiana kutatua shida mbalimbali.
B. Bi. Nasaha ameweza kuwatatulia shida za kifamilia.
C. Wanafunzi wamejua kusameheana nyumbani.
D. Wanafunzi wameweza kuwaelekeza wenzao katika shule za upili.

39. Maoni ya mwandishi wa kifungu ni kuwa,
A. shule nyingi zimeendelea kutokana na hazina ya ufadhili.
B. elimu hufanikiwa tu palipo na mandhari bora shuleni.
C. mtu anapodai haki hafai kujali hisia za wengine.
D. Haki inaweza kupatikana hata pasipo matumizi ya mabavu.

40. Kulingana na aya ya sita,
A. Tabia ya mtu huboreshwa kwa kushirikiana na walio wengi.
B. Uadilifu unaweza kumfanya mtu apuuzwe na wengine.
C. Ukitaka kujua uhalali wa jambo chunguza wanaolitenda.
D. Chanzo cha maovu yote katika jamii ni mazingira.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

*Yasome makala haya yanayofuata kisha ujibu maswali kuanzia nambari* **41** *mpaka* **50**

Ni wazi kuwa binadamu wote hawawezi kuwa sawa. Suala la tofauti za kitabaka limekuwepo tangu enzi za mababu zetu ambapo kulikuwa na koo za kifalme na nyingine za watumwa. Hata hivyo, suala hili limejitokeza zaidi kutokana na athari za kigeni na maendeleo ya viwandani ya teknolojia. Hili limewafanya akina mama wengi kutojikita katika kazi za nyumbani na kuajiriwa amali za ofisini au kujiajiri wenyewe. Hivyo basi pamekuwepo haja ya kuwaajiri mayaya wa kuwalinda watoto. Jambo hili linaendelezwa zaidi katika nchi changa barani Afrika kuliko ilivyo katika mataifa yaliyoendelea.

Hongera kwa mfumo wa elimu ya bure kwa watoto wa shule za msingi za umma na zile za upili za kutwa. Watoto hasa wa kike waliokuwa wakiajiriwa kazi za nyumbani hapo awali kwa sababu ya kutoweza kuenda shuleni wameweza kujiunga na shule. Idadi ya wasioenda shule imepungua kabisa. Hata hivyo msaada huu haufai kushughulikia shule za msingi na zile za upili kutwa tu. Kwa hivyo tatizo la kuajiri watoto lingalipo kwa kuwa wengi wanaajiriwa wangali katika umri wa chini ya miaka kumi na minane. Kulingana na sheria za taifa, hawa ni watoto wasiokuwa na vitambulisho na basi hawafai kuajiriwa popote. Janga la ubawinde nchini Kenya linawashirikiza watoto kutoka nyumbani ili kutafuta ajira hizi ili angalau wapate riziki badala ya kuwa miongoni mwa watoto wa mitaani au 'chokoraa' kama wanavyojulikana.

Kwa kawaida ujira wanaopata watoto hawa ni wa hali duni ikilinganishwa na kazi nyingi wazifanyazo. Wengi wao ndio majimbi majumbani na wao ndio wa mwisho kulala. Ndio wanaofagia, kupiga deki, kufua, kupiga pasi, kupika na hata kuandika meza huku akina mama watajiri wakiwa "wameandika nne" wakisoma magazeti. Hata baada ya kukipika chakula hicho baadhi ya watoto wanabaguliwa, wanaachiwa makombo au kutakiwa kula chakula wakiwa jikoni.

**Kila binadamu huhitaji muda wa mapumziko lakini sivyo ilivyo kwa watoto hawa.** Wengi wao kufanya kazi kwa muda usiopungua saa kumi na nane kwa siku. Ingawa sheria inayoshughulika na haki za wafanyakazi inasema kuwa waajiriwa wote wapewe siku moja kwa juma ya mapumziko, waajiri wengi hupuuza tu. Wengine hata hunyimwa haki ya kuabudu. Hawana nafasi ya kuhudhuria ibada.

Baadhi ya waajiri wa watoto hawa hawawalipi mishahara yao. Kwa makubaliano kati ya mwajiri na mzazi, pesa hizo zinapelekewa mzazi kila mwisho wa mwezi ilhali mhudumu hafaidi chochote. Waajiri wengine hutaka huduma ya bure na kujidai kuwawekea watoto hawa pesa zao ili liwe fungu kubwa ndipo wawape. Lakini wanapochoka nao huwafurusha mikono mitupu. Watoto hawa basi wanaendelea kusagika kwa kazi huku **kupe** wakifaidi.

Waajiri wanapaswa kuwafikiria wafanyakazi wale kama watoto wao ambao hawakubahatika kuenda shuleni na kuhitimu. Wengine ni mayatima wasiokuwa na mwingine yeyote wa kuwaonyesha huba la mzazi. Wengine hawakuendelea na masomo ya juu kutokana na matatizo mbalimbali ya kijamii. Kwa hivyo, haihalisi kuwapimia watoto hawa vyakula. Wakumbuke kuwa mayaya hawa ndio wanaowatunza watoto wao na kuwaandalia vyakula. Maisha ya wana wa waajiri hawa kwa kweli yamo mikononi mwa mayaya na kama wangeamua kuwatendea kinyama kama vile kuwapiga na kuwatukana, hali yao ingekuwa vipi?



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

41. Kulingana ya aya ya kwanza, binadamu
A. hawaweza kutosheka.
B. hawawezi kulingana.
C. hawawezi kufanana.
D. hawafai kuwa sawa.

42. Katika enzi za zamani,
A. kulikuwa na watu waliowatumikisha wengine.
B. hapakuwa na tofauti za kitabaka.
C. watu walikuwa na viwango sawa za mapato.
D. watoto wengi hawakuruhusiwa kufanya kazi.

43. Mwandishi anasema kuwa haja ya kuwepo mayaya limechangiwa na nini?
A. Wanajamii kutajirika na kuhitaji wafanyakazi.
B. Umaskini uliokita mizizi katika mataifa jirani.
C. Akina mama kujihusisha katika shughuli za kiuchumi.
D. Kuongezeka kwa majukumu kutokana na wingi wa watu.

44. Maana ya **nchi changa** kwa mujibu wa makala ni, nchi
A. zenye wananchi wengi wachanga.
B. ambazo ni ndogo kimaeneo.
C. iliyo na viwango vya juu vya umaskini.
D. ambayo inakua lakini haijajiimarisha vizuri kiuchumi.

45. Mojawapo ya changamoto zinazoukabili mfuno wa elimu ya mahonyo ni:
A. sio watoto wote wanaoruhuriwa kujiunga na shule.
B. udhamini huo unabagua watoto katika baadhi ya shule.
C. wanafunzi wa kike hawapewi nafasi ya kujiunga na shule.
D. shule zimekuwa nyingi za kushindwa kukidhi mahitaji ya wanafunzi wachache waliopo.

46. Kwa mujibu wa makala haya, mtu anayeajiriwa hana budi,
A. kuonyesha kimaumbile kwamba umri wake ni miaka kumi na minane.
B. kuwa na kitambulisho kitakachobainisha hirimu yake.
C. kuwa amehitimu mafunzo kulingana na mfumo.
D. awe ameidhinishwa na mashirika yanayotetea haki za wafanyakazi.

47. Ni maelezo yapi **yasiyo** sahihi kulingana na kifungu?
A. Watoto wote wameitikia mwito wa serikali wa kujiunga na shule.
B. Wapo wazazi wanaochangia kudhulumiwa kwa watoto wao.
C. Uyaya ni kazi ya kijungujiko licha ya uchovu wake.
D. Wengi wanaoajiriwa kazi ya uyaya hawafanyi hivyo kwa hiari.

48. '**Kila binadamu huhitaji muda wa mapumziko lakini sivyo ilivyo kwa watoto hawa**' maana yake ni kuwa: watoto
A. wanaoajiriwa ni tofauti na binadamu wengine.
B. hawa hupewa haki kama watu wengine.
C. hawa hudhulumiwa haki kinyume na binadamu wengine.
D. hawa hawafai kupumzika kama binadamu wengine.

49. Waajiri wengine hudai kuwawekea waajiriwa ujira ili wawalipe pesa nyingi baadaye. Ni methali gani inayogaa kuwasuta waajiri hawa?
A. Haba na haba hujaza kibaba.
B. Mchumia juani hulia kibaba.
C. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.
D. Heri kenda shika nenda kuliko kumi nenda rudi.

50. Neno **kupe** jinsi lilivyotumika lina maana gani?
A. mtu anayefurahia kuwatumikisha wengine.
B. mtu anayejifaidi kwa jitihada za wengine.
C. kiumbe anayeishi kwa kufyonza damu ya wengine.
D. kiumbe anayenyonywa jasho lake na wengine.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com